KATA YA LURAMBI MASHARIKI
DARASA LA NNE MUHULA WA PILI - 2015
KISWAHILI: LUGHA

JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU

1. Tumia penseli ya kawaida tu.
2. Hakikisha umeandika kwa karatasi ya majibu:-
   (i) JINA LAKO (ii) JINA LA SHULE YAKO

Muda: 1:40

Kamilisha kifungu hiki kwa kujaza mapengo kikamilifu

Mafuriko __1__ kutisha kabisa __2__ mwisho __3__ mwaka wa elfu mbili na nne. Wengine waka __4__ ita kabobo na wengine wakasema jina ni tsunami. Mafuriko __5__ yalikuwa __6__ kuliko __7__ ambayo ulimwengu umewahi kushuhudia maishani. Sababu ni mtetemeko mkubwa __8__ ardhi uliosukuma maji __9__ bahari hadi kuvuka kufikia nchi __10__.

1.	A. wa	B. za	C. ya	D. la
2.	A. uliotokea	B. zilizotokea	C. ilitoeka	D. yalitokea
3.	A. wa	B. ya	C. la	D. mwa
4.	A. u	B. zi	C. ya	D. i
5.	A. hiyo	B. huo	C. hizo	D. hayo
6.	A. kubwa	B. mikubwa	C. mkubwa	D. makubwa
7.	A. yote	B. zote	C. wote	D. kote
8.	A. za	B. wa	C. ya	D. la
9.	A. ya	B. za	C. la	D. wa
10.	A. mkavu	B. kukavu	C. kavu	D. mikavu

Jibu maswali yafuatayo kulingana na maagizo

11. **Kanusha sentensi hii:**
    Wewe umefika
    A. Wewe haujafika B. Wewe hukufika
    C. Wewe hujafika D. Wewe ulifika
12. Mmea unaozaa ndizi huitwa _____
    A. mhindi B. mndizi C. mti D. mgomba
13. **Andika wingi wa sentensi hii:**
    Huo ni mkate wako.
    A. Hiyo ni mikate yako
    B. Hiyo ni mikate yenu
    C. Hiyo ni mikate zenu
    D. Hizo ni mikate zenu
14. **Andika kinyume cha neno lililopigwa mstari**
    Mgeni alikutana na _____ wake.
    A. baba B. adui C. mwenyeji D. mama
15. Umbo hili ni _____



    A. pia B. mche C. mche mraba D. duara
16. Sisi kwetu tunakuna nazi tukitumia ____
    A. buli B. mbuzi C. mchi D. seredani
17. _____ ni kukata nyasi au magugu kwa kutumia kifyekeo.
    A. Kufyeka B. Kulima
    C. Kupanda D. Kupiga matuta
18. Neno **mtoto** liko katika ngeli gani?
    A. KI - VI B. LI - YA
    C. A - WA D. U - I
19. Mtu akikuambia **pole** utamjibu je?
    A. Nimeshapoa B. Niko
    C. Asante D. Salama
20. Andika tarakimu hii 1001 kwa maneno.
    A. Elfu moja na kumi
    B. Elfu moja na moja.
    C. Elfu mia moja na moja.
    D. Mia moja na moja
21. Ugonjwa wa kulala unaoambukizwa na mbung'o huitwa _____
    A. majipu B. malale C. kifafa D. kichocho

Tegua kitendawili

22. Nina mtoto wangu ambaye kila nikimwogesha hakauki ___
    A. sabuni B. kalamu
    C. ulimi D. picha

Kamilisha methali

23. Panya wengi hawachimbi _____
    A. barabara B. baraka
    C. nyumba D. shimo

24. Mtoto wa mwanangu nitamwita _____
A. mpwa B. kitukuu C. binamu D. mjukuu
25. Rangi ya mbingu ni _____
A. kijivu B. samawati
C. nyeupe D. nyekendu
26. Hiyo ni mikate _____.
A. yenu B. vyenu C. zenu D. wenu
27. Jua huchomoza kutoka upande wa _____ na huzama upande wa 28. _____

Andika kwa wingi
29. Mimi ninakula chakula kitamu.
A. Sisi tunakula chakula kitamu.
B. Sisi tutakula chakula kitamu.
C. Sisi tunakula vyakula vitamu.
D. Sisi tunakula chakula vitamu.
30. **Chagua kiulizi sahihi:**
Mkarakara ni mmea _____?
A. mgani B. yupi C. migani D. gani

Soma kifungu kifuatacho kisha uyajibu maswali 31 - 40

Magonjwa ni maradhi. Magonjwa mengine yanatupata kwa sababu ya makosa yetu na uzembe wetu. Maana yake ni kwamba, tukijihadhari na kujikinga, magonjwa mengine hayawezi kutupata. Baadhi ya magonjwa ambayo hayawezi kutupata tukichukua tahadhari na kujikinga ni kama yale maradhi ya Ukimwi, kichocho, malaria, homa ya matumbo, kipindupindu, kuendesha na mengineyo. Kwa hivyo, njia salama ya kupunguza au kuzuia magonjwa ni kujichunga, kuwa safi daima na kunywa maji safi. Kumbuka, kinga ni bora kuliko tiba.

31. Jina jingine la magonjwa ni _____
A.ugonjwa B. maradhi C. makosa D. upele
32. Ni nini kinachotusababisha kupatwa na magonjwa?
A. Makosa yetu B. Uchoyo
C. Uzembe wa wengine D. Hatujaambiwa
33. Magonjwa mengi hayawezi kutupata tukifanya nini?
A. Tukijikinga mvua
B. Tukijikinga na kutahadhari
C. Tusipotahadhari
D. Tukitibiwa
34. Magonjwa yapi hayawezi kutupata tukitahadhari?
A. Kichocho na ukimwiB. malaria peke yake
C. upele na vidonda D. Sijui
35. Kipindupindu ni ugonjwa wa _____
A. kuchezea B. kuumwa na kichwa
C. kuhara na kutapika D. usiotibiwa
36. Njia ipi siyo salama ya kuzuia magonjwa?
A. Kunywa maji safi B. Kuwa safi daima
C. Kujichunga D. Kuwa mchafu
37. Malaria ni ugonjwa unaosababishwa na ___
A. nzi B. mbu C. siafu D. kunguni
38. Nani anayetibu wagonjwa hospitalini?
A. Daktari B. Askari
C. Polisi D. Mwuguzi
39. Kinga ni bora kuliko _____.
A. afya B. tiba C. kinga D. ugonjwa
40. Kichwa kinachofaa zaidi ni _____.
A. Tiba B. Magonjwa
C. Homa D. Usafi

Soma hadithi ifuatayo kisha ujibu maswali kutoka 41 - 50

Siku moja ndama alimdunga shibli kwa pembe zake akamwua. Ilikuwa bahati mbaya tu. Walikuwa wakicheza, ajali ikatokea. Ajali haina kinga. Ndama aliogopa sana. Wazazi wao waliporudi kutoka kutafuta chakula ndama alikimbia haraka sana kwa mama yake. Akamweleza kuhusu ajali iliyotokea wakati wa mchezo. Ng'ombe alijua hasira za simba. Akamwambia mwanawe watoroke kabla simba hajajua kuwa mtoto wake ameaga dunia.

41. Kulingana na hadithi, nani aliyemdunga mwingine?
A. Shibli B. Ng'ombe C. Ndama D. Simba
42. Ndama ni kikembe cha _____.
A. simba B. ng'ombe C. shibli D. sijui
43. Ajali haina _____.
A. kinga B. dereva C. magari D. simba
44. Ni nani aliyemwelezea mzazi wake kitendo kilichotokea?
A. Shibli B. Ng'ombe C. Simba D. Ndama
45. Wazazi wao walirudi kutoka wapi?
A. Kutafuta pesa B. Kutafuta majani
C. Kutafuta chakula D. Hatujaambiwa
46. Nani aliyeaga dunia kulingana na hadithi hii?
A. Simba B. Ndama C. Shibli D. Ng'ombe
47. Kuaga dunia ni _____.
A. kusahau B. kufarikiC. kuamka D. sijui
48. Je ni nani aliyemtorosha mwanawe?
A. Ng'ombe B. Simba C. Shibli D. Ndama
49. Simba hujulikana kama _____ wa wanyama.
A. moto B. mfalme C. komando D. mkali
50. Hadithi hii haijamhusisha nani?
A. Simba B. Shibli C. Fisi D. Ndama

TARAFA YA MATHIOYA **DARASA LA NNE**

JARIBIO LA MTIHANI **MUHULA WA KWANZA - 2008**

KISWAHILI INSHA

MUDA: DAKIKA 40

Andika insha ya kusisimua juu ya kichwa ulichopewa.

DARASA LETU